



**MUKTADHA  
HAUPATIKANI**

**MUKTADHA HAUPATIKANI** - *UWEZO WA TASWIRA  
KUTEKELEZWA NA HUMBOLDT FORUM KAMA  
SEHEMU YA MAONESHU YA HISTORIA ZA TANZANIA.*

WASANII :  
CHARITY ATUKUNDA, LIZ KOBUSINGE,  
GLORIA KICONCO

WAFASIRI :  
ELIZABETH MAHENGE, JASMIN MAHAZI

VYANZO VYA PICHA :

STAATLICHE MUSEEN ZU BERLIN, ETHNOLOGISCHES  
MUSEUM, BILDARCHIV DER DEUTSCHEN  
KOLONIALGESELLSCHAFT, UNIVERSITÄTSBIBLIOTHEK  
FRANKFURT AM MAIN

# WAKESHA (na maiti)

WAPENDWA WAFIWA,

TUMEKUSANYIKA HAPA KUCHUNGUZA  
MAJERAHA YA KIKOLONI, KIFO CHA  
KUTOKANA NA MIKATO ELFU

KILA MKATO ULICHANJA NA KUCHONGA  
PICHA TOFAUTI, PICHA AMBAYO  
INABADILISHA HISTORIA YETU NA PIA  
WAKATI WETU WA LEO

KILA PICHA INABADILISHA  
TUNAVYOTAZAMWA NA  
TUNAVYOJITAZAMA WENYEWE,  
PIA NAMNA TUNAVYOTENDWA NA  
TUNAVYOJITENDEA WENYEWE

MAUMIVU YANAHIITAJI NAFASI  
YAKUJIELEZA, YA KUSIMULIA  
HADITHI YAKE

ULINDE MOTO ...



MALIGHAFI



PAMBA HUTENGENEZA KANGA,  
HUTUMIA TASWIRA KUTUPA  
HISTORIA NA HEKIMA KWA MANENO  
YAKE.


MKONGE UKASAFIRISHWA KIMAGENDO  
NDANI YA TUMBO LA MAMBA  
ALIYEKAUSHWA,  
MAZAO YA KIBIASHARA YA  
UJERUMANI, WAITA DHAHABU  
YA KIJANI.



**KUMBUKUMBU**

WAJERUMANI WAONAPO BIDHAA NA FAIDA  
YA KIUCHUMI

WATANZANIA HUONA YALE AMBAYO  
HUWAUNGANISHA



KINJEKETILE AFANYA DAWA YA  
MAJI MATAKATIFU, KWA KUTUMIA  
MAFUTA YA MNYONYO NA MTAMA

KUWALINDA WAPIGANAJI DHIDI YA  
RISASI.

WAUNGANA CHINI YA MKARAFUU,  
KUREJESHA UHURU WAO, ARDHI,  
NA NAFKA.

# SHIGANGA JILIKENYA

SHIGANGA JILIKENYA KU MABALA  
BAJELEMANI NA BAENGELEJA  
BALIKILING'HIMYA N'HAMBO  
LINGUNO YA NG'OMBE (2×)  
LILONGIJE  
LIKUBE, LIMULUNGU, BABA  
LIKATABI (2×)

LILIGOTOLA BANHU  
SIMBA SANA, NG'WANA MAKOMA  
NHOBOLA YABI YA BANGI  
YA MABILIJU, BABALYA BANHU! (2×)  
SHIGANGA JILIKENYA KU MABALA  
BAJELEMANI NA BAENGELEJA  
BALIKILING'HIMYA N'HAMBO  
LINGUNO YA NG'OMBE



TASWIRA ZA UKOLONI ZIMEPINDISHA  
MTAZAMO WETU WA MWAFRIKA NA  
WA MAZINGIRA YAKE NA HUMPOKA  
MUKTADHA NA UELEWA WAKE.

HUU MTEGO WA KIFIKRA  
WAJIRUDIA KILA WAKATI.

IKIWA TASWIRA YETU YA AFRIKA  
IMEJENGWA KWENYE UONGO,  
BASI INABIDI TUBADILISHE FIKRA ZETU  
UONGO UNAHITAJI KUONDOLEWA  
ILI MSINGI UJENGWE UPYA.

WAZIKA ULICHOFIKIRI WEWE WAKIJUA  
WAPUUZA HISTORIA ILOANDIKWA NA  
WAKOLONI NA WATEGAMASIKIO  
KUUSIKILIZA WASILISHO LA HISTORIA WA  
WAAFRIKA WENYEWE.

NDIVYO UTAKAVYOTOROKA  
MTEGO WA KIFIKRA

**MAZISHI**

# ARDHI

HUU SIYO UWANJA WA  
MICHEZO, NI ARDHI YA MTU.

KAMERA INADANGANYA KUKUONESHA  
UKIONACHO.

ARDHI INAONEKANA ITUPU, YAONESHA  
YASUBIRIA KUJAZWA.

NI WITO WA UONGO: "NJOO UCHUKUE  
ARDHI TUPU" AU KUMWAMBIA MWINDAJI:  
"NJOO UWINDE WANYAMA WA KIGENI".

MPIGAPICHA AFICHA DAMU YALOMWAGWA  
NYUMA YA FREMU.

PICHA ZINAUNDA NIA POTOVU. WAFURAHIA  
KUPORA NYUMBA ZA WATU.

PICHA ILOPIGWA YAENDELEZA MDUARA.  
WADHANIA ARDHI I TUPU NA UMEKUJA  
KUIJAZA.

UWAKUTAPO WATU, WAONDOE MWANZO ILI  
UWEZE KUIJAZA TENA ARDHI. KULAZIMISHA  
UKWELI UTAWALE FIKIRA ZAKO.

WAKATI WA KUDHALILISHWA,  
WAHANGA WAAMBWA WAVUE  
NGUO ZAO.

MMWILI

PICHA MOJA WAMEVAA NGUO:  
NYINGINE NGUO ZI CHINI MIGUUNI.



BAADHI HUANGALIA PEMBENI KUFICHA  
UDHALILISHWAJI, WENGINE WAANGALIA  
KWA KUTOJALI.



PICHA ZAPIGWA ANGALIA-MBELE NA  
ANGALIA-PEMBENI, KAMA PICHA ZA VIKOMBE,  
WANASAYANSI WAAINISHAPO SPISHI.



PICHA ZILIZOPIGWA HUUTUMWA, BILA JINA,  
BILA HISTORIA.

USICHOKIONA NI MIJEREDI YA KIBOKO.

LAKINI WAVEZA ISIKIA, ATHARI YA NYAKATI,  
KATIKA UPINZANI, NA MTAZAMO WA KUJIHAMI



HATUKUWARUHUSU  
KUTUKODOLEA  
MACHO

KUIREKODI  
MIILI YETU KWA  
MILELE .




TWADAI  
HESHIMA NA UTU  
WETU.

SASA, MTASIMULIAJE  
HISTORIA HII?  
BILA KUTONESHA  
MAJERAHA?




# NAMNA YA KUENDELEZA UCHU WA KIKOLONI

1.  
JIDANGANYE  
MWENYEWE




JIAMBIE MWENYEWWE WEWE NI  
MHUSIKA KWAMBA UMEKARIBISHWA  
HAPA. VUNJA KITI KWENYE MIGONGO  
YETU KANYAGA SHINGO ZETU KWA  
BUTI ZAKO.



JIDANGANYE  
UKIULIZWA: NI NINI  
KILICHOKULETA HAPA?  
SIYO MASHAMBA,  
VIWANJA NA MIGODI,

JE, SIYO FAIDA YA  
KIBINAFSI AU KUMPIGA  
KAKA YAKO,  
MWINGEREZA.



TUITE VITISHO,  
MPATE KUTUFUNGIA NDANI  
MDHIHAKI TUNACHOKIABUDU JIVISHE  
TAJI LA KUTUTAWALA UTUTEKE  
KWA KUTUGAWA.






VUNJA MIKUSANYIKO  
YETU MTUPONDE MPAKA  
TUREKEBIKE



TUFUNGIE MAHALI  
TUSIWEZE KUTENDA TUMIA  
WEUPE WAKO NA USOMI.






2.  
WADANGANYE  
NA WENGINE

WADANGANYE  
MKIULIZWA: KILICHOWALETA HAPA,  
KWA ARDHI NI KITU GANI  
KIMEWAPENDEZA?  
WAAMBIE ARDHI NI BIKIRA  
YA KWAMBA HAIKALIWI NA WATU.






WAAMBIE MMEKUJA  
KUSTAARABISHA KWA  
KUTUMIA BIBLIA, SARAFU  
NA BUNDUKI,

IKIWA KWELI MMEKUSUDIA  
KUFANYA UNYAMA KWA  
KUTUMIA BIBLIA, SARAFU NA  
BUNDUKI.

UTATU  
MTAKATIFU



CHAGUA MNACHOKISEMA  
KATIKA BARUA MUPELEKAZO  
NYUMBANI, KUWATANGAZIA UWONGO.  
KUUNDA MAKOLONI KUTOKANA NA  
UFALME, KWA KUTUFUKUZA MEKONI  
NA NYUMBANI MWETU.






CHORA MISTARI  
PALIPOKUWA NA  
FRAKTELI, CHORA  
MIPAKA YA  
MKANGANYIKO.



PIGA PICHA  
ZISIZO NA MAANA,  
TUONDOE KWENYE MUKTADHA  
WETU.



3.  
WATENGE WALE  
MLIOWADANGANYA




PATA ASHIKI KWA  
KUCHUNGULIA UCHI WA  
MTU, KWA KUTUINGILIA  
FARAGHA ZETU.

TUVUE NGUO MBELE  
YA KAMERA, TUFANYE  
MAHABUSU KWA PICHA  
ZAKO

VUKA MIPAKA  
YETU YOTE USIRUHSU  
TUSIMULIE HADITHI  
ZETU.





TUIBE SISI, ARDHI ZETU,  
MAZAO YETU TUGEUZE  
KUWA WANABANDIA

KUUA, KUNG'OA  
NA KUUZA KWENU  
ITATUGEUZA KUWA  
BIDHAA



MPATE KUSEMA NDIYO  
UKWELI WETU





ISIFU KABILA MOJA  
UDUMISHE JINGINE  
TUFARAKANISHE. WEWE KUWA  
MWENYE KUANDIKA SIMULIZI  
UWEKE MTAZAMO WAKO.



SISI NI TEMBO  
NA TEMBO KATU HASAHAU,  
LAKINI APUUZAYE  
KUMBUKUMBU ZAKE  
ATAKANYAGWA ANGALAU MARA  
MBILI.

